# OFISI YA RAIS –TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI MWAKIPESILE,
S L P 4689,
**MBEYA.**
Mob 0756215799 AU 0768952157
07/12/2020

Kumb Na MWSS/JOIN/VOL I/2021
JINA LA MWANAFUNZI____________________,
S L P______,
**MBEYA.**

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAKIPESILE WILAYA YA MBEYA MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021,** Shule ya sekondari Mwakipesile ipo umbali wa **km 50** kaskazini/mashariki/magharibi/kusini mwa mji mkuu wa Mkoa/Halmashauri ya wilaya ya **Mbeya.**

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/01/2021** ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

(a) Sare za shule
(b) Rangi ya sare
(c) Sare ya michezo
(d) Chakula cha mchana cha mwanafunzi

# SARE YA SHULE

**(a) WAVULANA**

- (i) Suruali mbili rangi ya kaki moja na kijani moja (usitumie mshono wa jinsi)
- (ii) Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- (iii) Soksi nyeusi
- (iv) Kiatu cha kamba cheusi
- (v) Sweta rangi ya kijani
- (vi) Tai mbili rangi ya kaki moja na rangi ya kijani moja

**(b) WASICHANA**

- (i) Sketi mbili rangi ya kaki moja na rangi ya kijani moja (mshono wa linda boksi)
- (ii) Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- (iii) Soksi nyeupe
- (iv) Kiatu cha kamba cheusi
- (v) Sweta rangi ya kijani
- (vi) Tai mbili rangi ya kaki moja na rangi ya kijani moja

# SARE ZA MICHEZO

**(C) WAVULANA**

- (i) Tsheti nyekundu
- (ii) Bukta nyekundu
- (iii) Soksi nyekundu
- (iv) Raba ya michezo

**(d) WASICHANA**

- (i) Tsheti nyeupe
- (ii) Tracksuit brue bahari
- (iii) soksi nyeusi
- (iv) Raba ya michezo

## ZINGATIA YAFUATAYO

(i) Hakikisha unakuja na fomu hii siku ya kuripoti
(ii) Hakikisha unajaza fomu ya uhakiki wa afya
(iii) Hakikisha unajaza sehemu zote muhimu
(iv) Hakikisha umesajiriwa kwenye kitabu maalumu cha wanafunzi.
(v) Hakikisha unanunua daftari kubwa (counter book) zisizopungua **kumi(10)**,kalamu, penseli na mkebe wa hesabu.

Kuchelewa/kutofika kwako kwa tarehe iliyopangwa kutasababisha nafasi yako kupewa mtu mwingine na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi wako.

3.0Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;na
i) Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au kusimamishwa Shule

a) Wizi.

b) Uasherati na ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika

e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau Bendera ya Taifa.

h) Kuwa mjamzito / kupata mimba.

h) Kuoa au kuolewa.

i) Kutoa mimba.

j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi.

l) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL
ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MBEYA DISTRICT COUNCIL

MWAKIPESILE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 4689,
MBEYA.

The Medical Officer,
..............................
..............................
..............................

**PARTI "A"**

Mr/ Miss..........................................................................................................

Please examine the above named pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories:-

1. Haemoglobin..........................................................................................
2. P.V. Bleeding..........................................................................................
3. Sight..........................................................................................
4. Blood pressure..........................................................................................
5. Urine for sugar and pregnancy tests..........................................................................................
6. Stool for routine examination..........................................................................................
7. Asthma......... ..........................................................................................
8. Skin diseases..........................................................................................
9. Leprosy..........................................................................................
10. Any deformity..........................................................................................
11. Epilepsy..........................................................................................
12. Pulmonary tuberculosis..........................................................................................
13. Neurosis..........................................................................................
14. Beaneries diseases..........................................................................................
15. Other serious diseases..........................................................................................

**PARTI "B"**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/ unfit/ mentally fit/ unfit for a full schooling.
2. Other comments..........................................................................................

..........................................................................................

Date... ........ . ........... ............

.....................................
Signature

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

FOMU S.S.4
ANUANI YA MZAZI/ MLEZI

.............................................
.............................................
.............................................

TAREHE...............................

AFISA ELIMU WA MKOA,
S.L.P 256,
**MBEYA.**

K.K. AFISA ELIMU SEKONDARI WILAYA,
S.L.P 599,
**MBEYA.**

**YAH: <u>HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SEKONDARI YA KUTWA.</u>**

Mimi.....................................................................Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi........................................ ninayeishi katika kijiji cha ............................ kata ya ............................ Wilaya..................... Mkoa...............................mtoto wangu alisoma Shule ya Msingi ya .........................katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Ninakubali mtoto wangu asome Shule ya Sekondari Mwakipesile katika Kata ya Iyunga Mapinduzi kwa kufuata masharti yafuatayo:-

(i) Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli zote za kishule akikaa nyumbani kwangu tangu kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne bila kuleta usumbufu kwa Afisa Elimu Mkoa au Wizara kuhusu makazi ya mtoto.

(ii) Kwamba nitahakikisha sichangii kwa namna yoyote ile dhidi ya mtoto kuacha shule.

**Kukiuka kwa haya sheria ifuate dhidi yangu**

.................................
**SAINI YA MZAZI/ MLEZI**

**KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi..........................................niliyechanguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka...............hapa Mwakipesile Sekondari ninaahidi kuwa nitafuata sheria za Shule kama zilivyo ainishwa kwenye fomu hii. Kiapo hiki ni kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne.

.................................
**SAINI YA MWANAFUNZI**